STATE OF WASHINGTON
**DEPARTMENT OF CHILDREN, YOUTH, AND FAMILIES**
CHILD CARE SUBSIDY PROGRAMS (CCSP)

# Huduma ya Rafiki, Familia na Jirani ya Ulezi (FFN) ya Nyumbani / Barua ya Mlezi Ndugu inayosubiri

**Family, Friend and Neighbor (FFN) In-Home / Relative Pending Letter**

Tarehe: ___________________

___________________________
NAMBARI YA SIMU YA KITUO CHA MAWASILIANO CHA RUZUKU YA MATUNZO YA MTOTO

___________________________
NAMBARI YA FAKSI YA KITUO CHA MAWASILIANO CHA RUZUKU YA MATUNZO YA MTOTO

___________________________
NAMBARI YA MAOMBI YA MTEJA

Umeomba msaada shirika la Working Connections Child Care wa kukulipia huduma ya matunzo ya mtoto itakayotolewa ima na:

1. Mtu ambaye si ndugu (rafiki au jirani) atakayekuja nyumbani kwako ili kutoa huduma ya ulezi wa mtoto; au
2. Ndugu mwenye vigezo (mwanafamilia) atakayetoa huduma nyumbani kwake au ndugu mwenye vigezo atakayekuja nyumbani kwako kutoa huduma ya ulezi wa mtoto.

**Tafadhali soma na fuata maelekezo katika Sehemu ya 1 na Sehemu ya 2 ya barua hii.**

## Sehemu ya 1. Kabla malipo hayajaidhinishwa na mtoa huduma hajapewa kibali na Idara ya Watoto, Vijana na Familia (DCYF)

Watoa huduma **wote** ambao ni wanafamilia, marafiki, na majirani (FFN) **wanapaswa**:

1. Kuwa na miaka 18 au zaidi.
2. Kujisajili katika tovuti ya watoa huduma ya WA Compass kupitia dcyf.wa.gov/services/early-learning-providers/ffn. Hii inajumuisha kupakia nakala ya kadi halali ya Huduma za Jamii (SSC) na kitambulisho chenye picha kinachotolewa na serikali, kama leseni ya udereva, kitambulisho cha jimbo la Washington, au pasipoti.

Baada ya mapitio ya usajili, mtoa huduma atatumiwa maelekezo ya jinsi ya kujaza maombi ya Portable Background Check (PBC) kupitia MERIT.

**Kwa maswali, wasiliana na DCYF kupitia 1-866-482-4325 Chaguo #8.**

| **Asiyekuwa Ndugu**<br>Huduma ya ulezi wa mtoto inaruhusiwa nyumbani kwa **Mtoto** tu. | **Ndugu** (mwanafamilia kiukoo, kwa ndoa au kwa agizo la mahakama)<br>Huduma ya ulezi wa mtoto inaruhusiwa nyumbani kwa **Mtoa Huduma** au nyumbani kwa **mtoto** |
|---|---|
| Mtoa huduma si ndugu wa mtoto na ni:<br>a) Rafiki; au<br>b) Jirani wa mzazi husika. | Mtoa huduma ni ndugu wa mtoto na ni:<br>a) Kaka au dada mtu mzima anayeishi nje ya nyumba ya mtoto;<br>b) Bibi au babu (pia nyanya, babu mkuu, nyanya mkuu);<br>c) Shangazi au mjomba (pia babu na mababu);<br>d) Binamu (lazima akamilishe matakwa ya Afya na Usalama katika Sehemu ya 3) au<br>e) Wanafamilia wengine kiukoo, kwa ndoa au kwa agizo la mahakama. |
| | |
| | Ikiwa uangalizi upo katika **nyumba ya mtoa huduma**, mtoa huduma lazima ahakikishe watu wote wenye miaka 16 au zaidi, anaoishi nao wajaze maombi ya Portable Background Check. |

## Sehemu ya 2. Baada ya kibali cha DCYF.

Tarehe ya kuanza malipo ni siku ya kupokelewa kibali cha Portable Background Check cha mtoa huduma au tarehe ya hivi karibuni ya kibali cha Portable Backgound Check cha wanakaya.

Ili kustahiki malipo, watoa huduma wote wa FFN wanapaswa:

A. Kukamilisha, ndani ya siku tisini 90 za kwanza za tarehe ya kuanza malipo, mafunzo ya DCYF ya Ufuatiliaji wa Mahudhurio Kielekroniki. Pata taarifa za mafunzo kupitia dcyf.wa.gov/services/early-learning-providers/electronic-attendance-system/training au DCYF kuuidhinisha mfumo wako wa ufuatiliaji mahudhurio kielekroniki kupitia dcyf.wa.gov/services/early-learning-providers/electronic-attendance-system/training.

B. Kutumia mfumo wa ufuatiliaji wa mahudhurio kielekroniki kila siku ili kujaza muda wa kuanza na kumaliza huduma ya ulezi itolewayo kwa kila mtoto na kuwasilisha kumbukumbu za kielekroniki kwa DCYF kila mwezi kwa kutumia mfumo wa kielekroniki.

C. Kusasisha taarifa zao kwenye tovuti ya watoa huduma ya WA Compass na MERIT kama kuna mabadiliko ya majina yao halali, anwani, baruapepe na nambari ya simu.

D. Kusasisha kumbukumbu zao za Uchunguzi wa Kihistoria (inahitajika kila baada ya miaka 3)

## Sehemu ya 3. Matakwa ya ziada

Yafuatayo ni **masharti ya ustahiki wa ziada wa kuendelea** kwa ajili ya watoa huduma kulingana na uhusiano wao kwa mtoto na mahali ulezi unapofanyika:

| Watoa huduma ambao **Si Ndugu na Binamu**<br>Uangalizi wa mtoa huduma ambaye Si Ndugu unaruhusiwa katika **nyumba ya Mtoto tu.** | Watoa Huduma ambao ni **Ndugu** wenye vigezo<br>Huduma ya ulezi wa mtoto inaruhusiwa nyumbani kwa **Mtoa Huduma** au kwa **Mtoto.** |
|---|---|
| 1. Ndani ya siku 90 za kwanza za tarehe ya kuanza malipo, mtoa huduma anapaswa kukamilisha:<br>a) Mafunzo ya Afya na Usalama au kupata uthibitisho wa msamaha wa mafunzo ya DCYF kwa mujibu wa WAC 110-16-0025(2)(b). Mafunzo ya Afya na Usalama ya DCYF yanaweza kupatikana mtandaoni kupitia: dcyf.wa.gov/services/early-learning-providers/ffn;<br>b) Kamilisha mafunzo ya huduma ya kwanza ya mtoto mchanga, mtoto na watu wazima na uhuishaji wa utendaji wa moyo na mapafu (CPR).<br>c) Kujaza tarehe ya kumaliza mafunzo ya CPR/First Aid ya MERIT kupitia https://apps.dcyf.wa.gov/MERIT/Home Kutoa ushahidi wa mafunzo ya CPR/First Aid (kadi, cheti, barua ya mkufunzi).<br>d) Kumaliza mafunzo ya 'Infant safe sleep' wakati wa uangalizi wa watoto wachanga<br>2. Kushiriki ziara ya kila mwaka na DCYF License Exempt Specialist, katika nyumba ambayo uangalizi unatolewa. Ukiwa na nafasi, wewe, au mzazi mnahimizwa kuwepo. Dhumuni la ziara hii ni kuhakikisha mtoa huduma anatii masharti ya afya na usalama, anazingatia mazingira ya ulezi wa mtoto na miingiliano ya mtoa huduma pamoja na mtoto, na anajadili taratibu za afya na usalama.<br>3. Kamilisha angalau saa mbili za mafunzo ya Afya na Usalama ya kila mwaka yaliyoidhinishwa na DCYF. | 1. Pale huduma ya ulezi wa mtoto inapofanyika nyumbani kwa mtoa huduma ambaye ni ndugu, watu wenye miaka 16 na kuendelea ambao:<br>a) Wanaishi na mtoa huduma ambaye ni ndugu wanapaswa kusasisha taarifa zao za Uchunguzi wa Kihistoria (inahitajika kila baada ya miaka 3)<br>b) Wanapanga kuishi na mtoa huduma ambaye ni ndugu, wanapaswa kukamilisha mchakato wa Uchunguzi wa Kihistoria kabla ya kuhamia kwa mtoa huduma. |

Child Care Aware inatoa taarifa na rufani za bure, na za haki kwa familia zinazotafuta malezi ya watoto yenye leseni na ubora wa juu. Piga nambari 1-800-446-1114 au mtandaoni katika childcareaware.org.

Ili kupata matokeo ya uchunguzi wa kihistoria ya malezi ya watoto yenye leseni, historia za leseni, ripoti za ufuatiliaji, lugha zinazozungumzwa na mengineyo mengi, nenda katika: Uchunguzi wa Malezi ya Watoto katika findchildcarewa.org. Ikiwa huwezi kupata taarifa hizi mtandaoni, tafadhali wasiliana na ofisi yetu kwa nambari 1-844-626-8687 ili tuweze kukupatia taarifa hizo.

Unaweza kujua iwapo maendeleo ya mtoto wako ni mazuri au iwapo anahitaji mazoezi ya ziada ili awe tayari kwa ajili ya shule. Ili kufanya hivyo, unaweza kujaza kidadisi cha maendeleo ya ukuaji wa mtoto cha bure kwa kuwapigia Afya ya Familia Moja kwa moja kwa 1-800-322-2588 au nenda kwenye tovuti ya Parent Help 123 parenthelp123.org/child-development/help-me-grow-washington ili kujifunza zaidi kuhusu hilo.

Watoto wana haki ya msingi ya binadamu ya kuwa salama. Vitendo vya unyanyasaji na utekelezaji vinahatarisha usalama wa watoto kwa kuwaweka katika hatari ya kupata majeraha ya kimwili, kihisia na hata kifo. Kama unashuku mtoto fulani ni mhanga wa vitendo vya unyanyasaji na utelekezaji, piga nambari ya bure ya DCYF kupitia 1-866-END-HARM (1-866-363-4276).

**Tafadhali wasiliana na Kituo cha Mawasiliano cha Ruzuku ya Matunzo kwa Watoto ikiwa wewe, mzazi, una maswali yoyote kuhusu hatua zinazofuata au ustahiki wako wa kuendelea kupitia 1-844-626-8687.**
**Kama mtoa huduma wako ana maswali kuhusu mchakato wa kibali na masharti husika mtaarifu awasiliane na mtaalamu wake halali kupitia: 1-866-482-4325 #8 au barua pepe kwa dcyf.ffn@dcyf.wa.gov.**